

**TAARIFA YA MRADI WA SHAMBA LA KAHAWA NA MIGOMBA (CHITAMBARUS FARM) UNAOTEKELEZWA NA FAMILIA YA MKULIMA PETER DAMAS NGAHYI
KWA KIONGOZI WA
MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU
CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05-06-2018**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Tunayo furaha kubwa kukukaribisha pamoja na Msafara wote uliofuatana nao hapa Kijiji cha Mbangamao nasema karibu sana na ujisikie upo nyumbani.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Mradi wa shamba hili la kahawa ulianzishwa mwaka 2011 kwa kupanda kiasi cha miche 4,000 katika nafasi ya mita 2.5 kwa 2.5 Mpaka sasa shamba lina jumla ya miti ya Kahawa 8,100 na Migomba mashina 600 ambayo imepandwa kwenye eneo la ukubwa wa ekari 15 zenye Hati miliki ya kimila. Madhumuni ya kuanzishwa kwa shamba hili la kahawa ni kuongeza pato la familia. Shamba hili ni kielelezo cha Mashamba ya Kahawa yaliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga ambapo kuna jumla ya ekari 19,933.1 sawa na idadi ya miti 12,754,106.00

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Baada ya kuanzishwa kwa shamba mwaka 2011 limekuwa likipanuliwa kidogo kidogo kwa kuendelea kupanda miche mipya na kufikisha miche 8,100 iliyopo shambani hivi sasa. Shamba limepandwa mikahawa ya Arabika, aina mpya ya miche chotara inayotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa TACRI ambayo ina uwezo wa kuhimili magonjwa sugu ya kahawa kama vile kutu ya majani na chule buni ya kahawa.

Gharama za mradi huu hadi kufikia sasa ni Tshs. 60,000,000/= hii ikiwa ni gharama za awali za uanzishaji na gharama za matunzo hadi kufikia miche kuanza kuzalisha kahawa. Pia anapenda kuishukuru Benki ya CRDB kwa kumuwezesha kupata mtaji wa kuanzisha na kuendeleza mradi huu.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Uzalishaji wa kahawa katika shamba hili umekuwa ukiongezeka kila mwaka kulingana na ongezeko la miche na kukua kwa mikahawa,

Msimu 2015/2016 nilivuna kilo 2,527 na kunipatia kiasi cha Tshs. 9,594,000.00

Msimu 2016/2017 nilivuna kilo 2,853 na kunipatia kiasi cha Tshs. 15,530,000.00

Msimu 2017/2018 nilivuna kilo 6,237 na kunipatia kiasi cha Tshs. 24,513,830.00

Shamba pia lina uwezo wa kuzalisha ndizi kwa wastani wa mikungu 1,500 sawa na Tshs. 5,000 kwa kila mmoja na kunipatia Tshs. 7,500,000/= kwa mwaka.

Kutokana na pato hilo familia inaweza kumudu gharama za maisha na kuwekeza kwenye elimu ya watoto wangu kwani naamini Elimu ni ufunguo wa maisha na kuwekeza ni sasa. Malengo kwa yake ni kuongeza uzalishaji wa kahawa kwa mti wastani wa kilo 3 kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo. Kahawa inayovunwa kutoka kwenye shamba hili itauzwa kupitia chama cha Ushirika cha Msingi KALIME ili kupata faida zaidi.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Napenda kutoa wito kwa Wananchi wenzangu kuwa kilimo ni kazi ni ajira na ni biashara inayoweza kunipa kipato cha kumudu ghalama za Elimu kwa familia yangu na mahitaji mengine.

Pia nimeweza kuajili Vijana 15 ambao wanapata kipato kinachowawezesha kumudu maisha yao ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika Elimu kwani **‘Elimu ni ufunguo wa maisha,wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu’**.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Baada ya taarifa hii, kwa heshima na taadhima naomba ukague shamba langu.

Ni mimi,

DR.KESSAM MASWAGA
Kny;MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI.
MBINGA